

COUNTY GOVERNMENT OF LAMU



THE COUNTY ASSEMBLY OF LAMU

THE HANSARD

Wednesday, 27th April 2022

*The Assembly met at the
Main Chambers, at 10:30 AM*

[Temporary Speaker (MCA Amina Kale Loo) in the Chair]

PRAYERS

STATEMENTS

MCA Sheikh Abdallah Aboud: Thank you Madam Speaker. I raise to seek a statement pursuant to standing order 41(2)(C) from the chairperson on the departmental Committee on agriculture and Natural resources on matters relating to the County tractor.

I am aware that our County Government purchased tractors to assist subsidized farming and helping farmers at a cost of 1000 per acre.

Due to the drought situation, farmers have faced a lot of problems hence calling for an urgent attention to the County Government to wave.

Madam Speaker I seek to know from the chairperson of the departmental Committee on agriculture, Fisheries and Natural resources on the following matter:

1. Why can't the County Government be regulating Levi from sh.1000 to sh.500 per acre?
2. Is there any possibility the County Government to assist farmers on ploughing on credit based because of the collapse of the project?
3. When will the County Government send the new tractor to Kiunga ward?

MCA Anab Mohamed Hajj: Asante Mheshimiwa Spika, mimi pia nimesimama kuunga mkono. Ni kweli kuwa wananchi wako kwenye shida, hakuna ajira, kuna ukame na hakuna maji. Mimi naona ni vizuri tuweze kutilia mkazo waweze kupunguziwa kutoka hio elfu moja mpaka mia tano na pia ikiwezekana kama mtu hana pesa na ana uhitaji apewe nafasi alime kisha baadae akipata pesa atalipa kwani hii itaweza kusaidia jamii kuinuka katika maisha.

MCA Jonathan Baya Mketta: Mimi pia nimesimama kutilia mkazo na kuongezea ni kuwa tumethirika pakubwa katika jamii kwa sababu ya corona kote ulimwenguni na pia janga la ukame.

Mheshimiwa Spika serikali ya Kaunti imenunua tinga tinga ili kuinua ukulima kwa wakaazi wa Lamu na pia ikapunguza pesa za malipo ya kila ekari. Rai yangu mimi ni kuwa eneo langu la Witu liko na shida kama kwengine.

Mheshimiwa Spika umefilka wakati wa serikali ya Kaunti kuja kusaidia wananchi wake. Ikiwa bajeti imekuja na tumepitisha na tumenunua hizo tinga tinga, itakuwa vyema serikali ya Kaunti ichukue jukumu la kuwalimia hawa wakulima angalau ekari mbili mbili.

Vile vile, ni kitu gani serikali ya Kaunti itawafanyia wakulima ili wahisi kwamba wanafanyiwa haki na wawakilishi wao kuwafanyia maslahi yao.

Kwa hivyo ningepomba kupitia kwa ofisi yako hatua nzuri ichkuliwe kuhakikisha mwananchi amesaidika kwa hili.

MCA Zulekha Mohamed Mjahid: Mheshimiwa Spika mimi pia nimesimama kuongezea kwa sababu huku kwetu Lamu kuna mvua fupi na saa hii rasha la kwanza limeshapiga, likipiga la pili kama tinga tinga hatukulipata sisi watu wa Lamu mashariki tutaumia. Kwa hivyo twaomba serikali ya Kaunti itie mkazo wa kufikisha tinga tinga.

MOTION

MCA Festus Kihuha: Madam Speaker, I beg to move the following motion:

That pursuant to standing order 190(5)(F) This House adopts the approval of the report of the County public investment under County committee on the financial statement of

the Lamu County fisheries development fund for the year ended 30th June 2019 tabled on the floor of the House on 26th April 2022.

Seconded

Motion proposed

Members contribution

MCA Sheikh Abdallah Aboud: Asante Mheshimiwa Spika. Nimesimama kuunga hii hoja kwa sababu inahusu sana wavuvi wetu ambao walipewa mashini na Kaunti na kupitia bunge hili tuka wave na la kuskitisha serikali ya kaunti bado haijafuta hizo kumbikumbi katika rekodi na mara nyingi auditors wakija bado wanaifanya hio kuwa hoja kwamba hizi pesa hazijalipwa kwa hivyo kuna umuhimu wa serikali ya Kaunti kufuta kumbikumbi hizi.

Vile vile pesa zile ambazo zimelipwa wavuvi wale wanunuliwe vifaa ili waweze kuendelea na Kaunti isivasumbue tena katika mambo haya.

MCA Jane Ndung'u: Asante Mheshimiwa Spika mimi pia nimesimama kuunga hoja hii. Kaunti ya Lamu tumebarikiwa sana, tuko na wavuvi wa bahari maji chumvi na tuko na wale wa maji tamu. Sisi kama wenyeji wa wadi ya Bahari tuko na maskitiko makubwa kwa sababu samaki inayoshughukiliwa Kaunti ya Lamu ni wa baharini ilhali wale wa maji tamu wameachiliwa na hawapati vifaa na usaidizi wowote.

Mheshimiwa Spika naomba mambo yoter yatakayopatikana kwa wavuvi wa maji chumvi na wale wa maji tamu pia wapate.

Movers response

MCA Festus Kihuha: Mheshimiwa Spika nimesimama hapa kwa wale waloniunga kwa mswada huu. Mswada huu ukiingia utaweza kusaidia wavuvi ili waweze kununua vifaa vyengine ambavyo vitaweza kuwasaidia.

(Question put and agreed upon)

[Temporary Speaker (MCA Amina Kale Loo): Honorable Members, there being no other business, the Assembly stands adjourned until in the afternoon, 2:30 PM.

The Assembly arose at 10:45 am